KATIKA MAHAKAMA KUU TA ZANZIBAR
IMESIKILIZWA TUNGUU
RUFAA YA JINAI NAMBARI 103 YA 2024
(kutoka kesi ya jinai nambari 31 ya 2023, Mahakama ya Mkoa, Mwera)

AIMAN MOH'D MMEVELA.....MUOMBA RUFAA
VS
DPP.....MJIBU RUFAA

HUKUMU YA RUFAA

Date of Last order: 28.02.2025
Date of Judgment: 25.03.2025

S. A. HASSAN,J.:

Muomba rufaa alishtakiwa katika Mahakama ya Mkoa, Mwera kwa kosa la kubaka, kinyume na vifungu 108(1),(2)(e) na 109(1) vya sheria ya adhabu nambari 6/2018, Sheria za Zanzibar. Ambapo ilielezwa Mahakamani kuwa muomba rufaa mnamo tarehe 22.03.2022 majira ya saa nane mchana huko Koani, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja alimbaka AMA (jina linahifadhiwa) mtoto wa kike mwenye umri wa miaka kumi na sita, jambo ambalo ni kosa kisheria. Baada ya shauri kusikilizwa, Mahakama ya Mkoa Mwera ilimtia hatiani muomba rufaa na kuamuru atumikie Chuo cha Mafunzo kwa muda wa miaka kumi na mbili na alipe fidia ta Tsh 300,000. Kwa vile hakuridhika na hukumu na adhabu hiyo amekata rufaa Mahakama hapa akiambatanisha sababu kumi za rufaa ambazo kwa ujumla wake ameitaka mahakama hii ione mapungufu yaliyopo kwenye shauri mama na kuikubali rufaa yake.

Siku ya kusikilizwa rufaa hii, muomba rufaa hakua na uwakilishi na upande wa muobewa rufaa uliwakilishwa na Suleiman Fadhil na Hamad Mwalim, wote wakiwa ni mawakili wa Serikali.

Kwa vile muomba rufaa hakua na ujuzi wa maswala ya kisheria, aliiomba mahakama hii izizingatie sababu zake za rufaa kama alivyoziwasilisha. Na kwa upande wa majibu, upande wa Serikali ulijikita zaidi kwenye kesi ya **Suleiman Makumba Vs R [2006] TLR 379** kwamba ushahidi mzuri wa mashauri ya kubakwa huwa unatokana na muhanga mwenyewe, aidha shauri husika ni la kubakwa kwa msichana alie chini ya

umri wa kutoa ridhaa. Aidha, ilielezwa pia muhanga hakupiga kelele kwa sababu muomba rufaa alimtisha. Hata hivyo, Mahakama hii iliombwa iutupilie mbali ushahidi wa PW4 kwani unakinzana na maelezo ya mashahidi wengine. Mwisho kabisa, Mahakama imeombwa iitupilie mbali rufaa, adhabu na hukumu viendelee.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili, Mahakama hii inaona ni vyema kuzipitia kumbukumbu za shauri husika ili niwe kwenye nafasi nzuri ya kulitolea maamuzi shauri hili.

PW1 ambae ni muhanga alieleza kuwa siku ya tarehe 22.03.2022 saa nane mchana alikua na muomba rufaa ndani ya nyumba ambayo wote ni wa wapangaji na Aiman alimuingilia baada ya kumuita chumbani na kumkamata mkono na kumtisha na kumwambia avue nguo, lakini hakuvua ndipo muomba rufaa alimpomvua kwa nguvu na kumuingilia. PW1 aliendelea kueleza kuwa wakati yote hayo yanatokea, mama yake hakuwepo na aliporudi alianza kumtafuta na kumkuta ndani ya chumba cha muomba rufaa. Wakati akihojiwa, PW1 alieleza kuwa siku anaingiliwa na muomba rufaa hakupiga kelele kwa sababu muomba rufaa alimwambia asipige kelele, na kwamba siku hiyo ndio mara ya kwanza kuingiliwa na muomba rufaa lakini kabla ya hapo alishawahi kuingiliwa na mtu aliemtaja kwa jina moja la Haji na kwamba yeye muhanga hakuingia chumbani kwa muomba rufaa kwa hiyari na aliingia humo kuanzia saa nane mchana hadi saa kumi na mbili jioni. Aidha amesema pia muomba rufaa akitoka huwa anarudi usiku.

PW2 alieleza kuwa alipokea taarifa ya kutoonekana kwa muhanga kuanzia saa nane mchana hivyo alirudi kwake na kutoa rai ya kufanya msako chumba hadi chumba kwani nyumba ile wanaishi wapangaji wengine, na walianza kwenye chumba cha muomba rufaa, hivyo waligonga mlango walimkuta muomba rufaa hana shati na walipoangalia ndani walimuona muhanga amejiweka nyuma ya mlango, hapo PW2 alifunga mlango na kwenda kumuita sheha ambae alipiga simu polisi.

PW3 alieleza kuwa alipokea simu inayohusiana na tukio la udhalilishaji, alikwenda eneo la tukio na kukuta watu wengi wapo nje wamezongea chumba ambacho alikuwemo mtuhumiwa, mlango ulipofunguliwa walimkuta muomba rufaa amekaa peke yake kwenye godoro, hivyo alimuulizia muhanga akaambiwa yupo chumba cha pili, baada ya

hapo muhanga na muomba rufaa wote walichukuliwa kituo cha Polisi Dunga, na baada ilitolewa PF3 kwa ajili ya uchunguzi kwa muhanga.

PW4 ameeleza kuwa yeye ni mama wa muhanga, siku ya tukio alikua hayupo na alirudi saa kumi jioni na kukuta muhanga hajulikani amekwenda wapi hivyo aliwaarifu jamaa na majirani, na ilipofika saa kumi na mbili na dakika arobaini na tano jioni muhanga alionekana aloitoka kwenye chumba cha muomba rufaa. Aidha, alieendelea kueleza kuwa siku ya pili yake alikwenda na muhanga Hospital kwa ajili ya uchunguzi na daktari baada ya uchunguzi alimueleza kuwa muhanga hakuwa ameingilia siku hiyo ili alishawahi kuingiliwa kabla ya hapo. Shahidi PW4 pia alieleza kuwa tokea muomba rufaa aanze kuishi hapo hadi siku ya tukio ni wiki mbili tu na kwamba muomba rufaa akitoka kwenye nyumba huwa anarudiu usiku, aidha hakua na uhakika kuwa siku ya tukio muomba rufaa alikuwemo ndani ya chumba chake wakati muhanga anatoka, na kwamba aliemuona muhanga anatoka huko chumbani ni Ayoub, na kwamba chumba cha muomba rufaa wakati mwengine kinafungwa na wakati mwengine kinaachwa wazi kabisa.

PW5 ambae ni dakatari aliemfanyia uchunguzi wa kitaalamu muhanga, aliona kwenye utupu wa mbele hakuna kidonda wala michubuko, ila aliona mikatiko iliyopoa ila hakua na michubuko wala manii kwa siku alipofanyiwa uchunguzi.

Kwenye utetezi wa wake muomba rufaa alieleza kuwa yeye anafanya akzi ya kuosha magari hapo Koani na kwamba siku ya tukio hakuwepo hapo nyumbani na alirudi usiku, alioga na alipokua amejipumzisha alisikia mlango unagongwa na alipofungua alimuona mpangaji mwenzake akiwa na askari ambao walimchukua hadi kituo cha polisi hivyo yeye akamjuuliusha bosi wake kwani alipofika kituoni aliambiwa ana kosa la ubakaji. Aidha aliendelea kueleza kuwa baba wa muhanga alimtaka muomba rufaa ampe tsh 5,000,000 ili kesi iishe.

DW2 amabe ni mfanyakazi mwenzake muomba rufaa alieleza kuwa siku inayodaiwa tukio kufanyika muomba rufaa alikua kazini kwake hivyo hawezi kufanya kosa ambalo anatuhumiwa nalo. Baada ya muomba rufaa kukamatwa, DW2 anaeleza kuwa askari mpelelezi aliwaambia kuwa kabla kesi yao haijafika juu wawatafute wazazi wa muhanga

ili kesi imalizike. Baada ya kuwafata wazazi wa muhanga, walidai wapatiwe Tsh 5,000,000 ili kesi iondolewe, ambazo tulisema hatuna na wakatwambia kesi itaenda juu. DW3 ambae ndie mmliki wa eneo la kuoshea magari anapofanyia kazi muomba rufaa alieleza kuwa muomba rufaa hufanya kazi ya kuosha magari siku nzima, na siku ya tukio alikuwepo kazii, na alipopata taarifa ya kukakamatwa kwake alifanya mawasiliano na baba wa muhanga amabe alitaka apatiwe Tsh 5,000,000 ili iwe mahari, ndipo aliposema kuwa yeye hana na ataangalia hatma ya Mungu.

Baada ya kupitia kumbukumbu za shauri mama, na kusoma hukumu ya Hakimu wa Mkoa, ni wazi kuwa shauri hili limeamuliwa kijuu juu sana licha ya umakini mabao unatakiwa kufanywa kwenye kuamua mashauri ya aina hii. Aidha, mahakama hii inasisitiza kuwa kuegemea kwenye shauri za **Suleiman Makumba** (imetajwa huko juu) na kutoa maamuzi kwa sababu tu muhanga amentaja mtu bila ya kujiridhisha kwa kina ni hatari sana kwani mara kadhaa mahakama zimeona sio kila anachokisema muhanga ni cha kweli. Mfano kwenye shauri hili muhanga anasema siku ya tukio aliingiliwa na muomba rufaa, lakini daktari aliemfanyia uchunguzi ameweza kuona mikatiko iliyopoa, maana yake kuwa ni kweli muhanga aliwahi kuingilia, lakini sio siku ambayo inasemekana aliingiliwa, kwani uchunguzi ulifanywa siku hiyo hiyo na daktari hakuona chochote kinachoashiria kuwa siku hiyo aliingiliwa, hivyo basi mahakama kusema kuwa maneno ya muhanga yanatosha kuthibitisha kosa, kwa upande wangu ninaona sio sahihi kwani maneno ya muhanga sio msahafu, na kwenye shauri hili imeonekana hivyo.

Aidha, kuuondoa ushahidi wa PW4 kwa vile unakinzana na maelezo ya mashahidi wengine, kwa upande wangu ninaona sio sahihi, kwani ukisoma maelezo ya mashahidi wa pande zote mbili, ni wazi kuwa ushahidi wa PW4 unauunga mkono ushahidi wa utetezi kuwa muomba rufaa huwa anatoka siku nzima, na pia chumba chake kuna siku kinafungwa na kuna siku kinakua wazi. Hivyo kukinzana kwa ushahidi wa PW4 bahati mbaya sana Mahakama ya Mkoa umeshindwa kuona kuwa ni jambo kubwa ambalo kama Mahakama hiyo ingeliupima vyema ushahidi huu basi maamuzi yake yasingelikua haya ambayo yamekatiwa rufaa hapa.

Aidha, Mahakama ya Mkoa haijaelezea kwa kina swala la muomba rufaa na jamaa zake kuambiwa watoe tsh 5,000,000, jambo ambalo mashahidi wote wa utetezi wamelielezea.

Kwa jicho la haki, ukipitia mtitiriko mzima wa shauri hili, ni rahisi kuona kuwa shauri mbele ya Mahakama ya Mkoa lilikua ni la kupangwa, hivyo hakimu angelifanya kazi yake kwa umakini unaotakiwa angeliweza kugundua hilo na shauri lisingefika hapa lilipofika. Hivyo basi Mahakama hii, inaikubali rufaa hii na kutengua uamuzi na amri zilizotolewa na Mahakama ya Mkoa na kuamuru muomba rufaa aachiliwe huru mara moja isipokua kama ameweka kizuizini kwa sababu nyengine za kisheria.

Inaamriwa hivyo.

S.A.HASSAN

JAJI

25.03.2025

Haki ya rufaa inaelezwa.

S.A.HASSAN

JAJI

25.03.2025